# Kenya: Wahusika wa Ghasia za Uchaguzi Mkuu Wahukumiwe

***Unda mahakama maaalum ya kutoa haki kwa waathiriwa***

(Nairobi, Desemba 9, 2011) – Miaka minne baada ya ghasia za baada ya uchaguzi mkuu mwaka 2007-2008 maafisa wa polisi wa Kenya na mahakama zimeshindwa kufanya uchunguzi kwa ukamilifu na kuwashitaki wahalifu na kuhakikisha kuwa haki inatekelezwa kwa waathiriwa wa ghasia hizo, shirika la Human Rights Watch limesema kwenye ripoti iliyotolewa leo. Ijapokuwa mahakama ya kimataifa ya uhalifu (ICC) inashughulikia kesi kadhaa, Kenya inapaswa kuunda mahakama maalum ili kuleta uwajibakaji, Human Rights Watch limesema. Inapaswa pia kutoa fidia kwa waathiriwa, kuanzia na waathiriwa 21 ama zaidi ambao walipigwa risasi na polisi na walioshinda kesi dhidi ya mwanasheria mkuu, lakini serikali imeshindwa kuwafidia baada ya mahakama kutoa agizo.

Ripoti hiyo yenye kurasa 95, "'Turning Pebbles:' Kuepuka Uwajibikaji kwenye Ghasia za Uchaguzi nchini Kenya," inachunguza jawabu ya polisi na mahakama kufuatia ghasia za uchaguzi ya mwaka 2007, ambazo zilizua vurugu baina ya wafuasi wa chama tawala na polisi dhidi ya makundi ya upinzani na raia. Shirika la Human Rights Watch liligundua kuwa kati ya visa vya mauaji 1,133 ama zaidi vilivyoyotekelezwa wakati wa ghasia hizo, ni viwili tu ambavyo hukumu ya mauaji imetolewa. Waathiriwa wa ubakaji, mashambulio, kuchomwa, na uhalifu mwingine pia wanasubiri haki itendeke. Maafisa wa polisi, walioua yamkini watu 405 wakati wa ghasia hizo, walijeruhi zaidi ya watu 500, na kubaka wanawake na wasichana kadhaa, hawajachukuliwa hatua yoyote.

"Maafisa husika wa Kenya wameahidi kila mara kuwa watachunguza na kuwahukumu wahusika wa ghasia za uchaguzi, lakini uhaba wa hukumu ni ishara ya ukosefu wa nguvu za kufuatilia," alisema Daniel Bekele, Mkurugenzi wa shirika la Human Rights Watch barani Afrika. "Kenya izishughulikie kesi hizo na mahakama maalum itakayokuwa na majaji na viongozi wa mashtaka wa kimataifa waliohitimu wala isiingiliwe kisiasa."

Msingi wa ripoti hiyo ni mahajiano yaliyofanyiwa watu 172 na tathmini ya faili 76 za mahakama zilizoko katika mikoa ya Nairobi, Bonde la Ufa, Magharibi, Nyanza, na Pwani.

Kiongozi wa mashtaka katika mahakama ya ICC amewasilisha kesi za washukiwa sita wakuu wanaotuhumiwa kwa uhalifu dhidi ya binadamu. Kesi hizo zimeendelea licha ya misururu ya hila za kisiasa na kisheria zinazofanywa na mamlaka nchini Kenya za kujaribu kuahirisha ama kuzuia hukumu kutolewa. Mahakama hiyo inatarajiwa kuamua iwapo kuna ushahidi wa kutosha kwa kesi hiyo kuendelea ifikapo mwezi januari mwaka 2012.

Mwanaharakati mmoja nchini Kenya aliliambia shirika la Human Rights Watch kuwa mahakama ya ICC ni "Taasisi ya kwanza [wanasiasa wa Kenya] wamekutana nayo ambayo hawewezi kutoa hongo, kuua ama kutisha," hivyo waathiriwa wengi wameanza kutumaini kuwa haki itapatikana.' Lakini mamia ya wahusika wa uhalifu mkubwa wanaendelea kuepuka uwajibikaji. Uhalifu huu unajumuisha zaidi ya mauaji 1,000 na visa 300 vya kutoweka ama kupotea katika eneo la Mt. Elgon nchini Kenya na ambalo pia linahusishwa na ghasia za uchaguzi.

Shirika la Human Rights Watch lilitambua ulegevu mkuu wa mfumo wa mahakama ambao umechangia idadi ndogo ya hukumu zilizotolewa. Maafisa wa polisi wamekuwa wakikataa kuchunguza na kuwahukumu wenzao, ubora wa uchunguzi umekuwa duni, na maafisa wengine wa polisi wanaoongoza mashtaka hawajahitimu, Human Rights Watch limesema. Muingilio wa kisiasa na ufisadi umeathiri utendakazi wa mahakama; na Kenya haina mfumo endelevu wa kuwalinda mashahidi.

Mzee wa jamii ya Kalenjin mjini Eldoret aliliambia shirika la Human Rights Watch, akizingatia uwajibikaji kwenye ghasia za baada ya uchaguzi, "Sisi ni wazuri sana kwa kusema hatutaacha jiwe lolote kama halijafurukutwa, lakini hatugeuzii jiwe lolote. Pengine tugeuzee kokoto.… vijiwe vidogo hugeuzwa. Yale makubwa, hakuna anayethubutu."

Shirika la Human Rights Watch liligundua kuwa ijapokuwa wahusika wengine walihukumiwa kwa makosa madogo, wale waliohusika kwa makosa makubwa na wote waliopanga ghasia hawajachukuliwa hatua yoyote- wamefidia hali ya kutojali.

Wito wa kuunda mahakama maalum nchini Kenya – mwanzo ulitolewa na Tume ya Waki iliyokuwa ikichunguza Ghasia za Uchaguzi mwezi Oktoba, mwaka 2008 – angali muhimu na wa dharura, Human Rights Watch limesema. Huo ni ukweli, ikizingatiwa matatizo ya uhuru na uhakika wa mfumo wa mahakama nchini, ushahidi ulioelezwa na shirika la Human Rights Watch, na kuwa huenda mahakama ya ICC ikashughulikia idadi ndogo ya kesi.

Bunge la Kenya na mawaziri mara kadhaa mwaka 2009 walipendekeza sheria ya kuanzisha mahakama maalum, lakini walishindwa kuipitisha. Desemba 15, 2010 – mwaka moja uliopita – rais Mwai Kibaki alitangaza, "Serikali imejitolea kikamilifu kuanzisha mahakama maalum kushughulikia wahuisika wa ghasia za uchaguzi, kwa mujibu wa katiba mpya." Tangu mwaka mmoja ukamilike, hakuna hatua madhubuti ambazo zimechukuliwa kuanzisha mahakama hiyo.

Kenya inapaswa kupiga hatua ya kuunda mahakama maalum huku ikiendelea kushirikiana na mahakama ya ICC, Human Rights Watch limesema. Mahakama hiyo itajaza mapengo yaliyoko iwapo haitaingiliwa na masuala ya kisiasa na kushirikisha wataalam wa kitaifa na kimataifa. Kenya inafaa pia kuongeza juhudi za kuboresha uchunguzi wa maafisa wa polisi na kuajiri raia waliohitimu kuwa viongozi wa mashtaka.

Serikali inafaa ifadhili mara moja shirika la kutoa ulinzi kwa mashahidi, ambalo lilizinduliwa mwaka 2011 lakini halijawahi kutoa ulinzi hata kwa shahidi mmoja. Inafaa ifidie waathiriwa ambao tayari wameshinda kesi dhidi ya serikali kwa kupigwa risasi na polisi wakati wa ghasia za uchaguzi. Serikali inafaa kutatua kesi zingine ambazo zinaendelea, na kuanzisha mfumo mzuri wa kuwafidia waathiriwa wa ukiukaji wa haki za binadamu.

"Chini ya sheria ya kimataifa, Kenya inalo jukumu la kuwahukumu wahalifu wakuu na waathiriwa wa uhalifu ule wana haki ya kutendewa haki," Bekele alisema. "Kutenda haki kwa waathiriwa ni lazima wala sio chaguo. Miaka minne baada ya ghasia, waathiriwa wamekuwa wakisubiri kutendewa haki kwa muda mrefu."

**Wakati huu ambapo kazi hii hairuhusu kuchapishwa, "'Turning Pebbles': Kuepuka uwajibikaji kwenye Ghasia za Uchaguzi nchini Kenya," inapatikana:**

http://hrw.org/embargo/node/103360?signature=2ff8a3861f23cdb80e431cd7d083e0ac&suid=6

**Ikishatolewa, itapatikana:**
http://hrw.org/reports/2011/12/09/turning-pebbles-0

**Kwa maelezo zaidi ya ripoti ya Human Rights Watch kuhusu ghasia za uchaguzi na uwajibikaji nchini Kenya, tafadhali tizama:**

- **"Ballots to Bullets: Kupangwa kwa Ghasia za Kisiasa na Mgogoro wa Utawala," Machi 2008,** http://www.hrw.org/reports/2008/03/16/ballots-bullets
- **"Unfinished Business: Kuziba Mianya kwa Uteuzi wa Kesi za ICC," Septemba 2011,** http://www.hrw.org/reports/2011/09/15/unfinished-business-0
- **"'Hold Your Heart': Kusubiri Haki katika eneo la Mt. Elgon nchini Kenya," Oktoba 2011,** http://www.hrw.org/reports/2011/10/27/hold-your-heart

**Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:**
Aliye Nairobi, Neela Ghoshal, (Kiingereza, Kifaransa): +254-729-466-685 (simu ya mkononi); ama ghoshan@hrw.org
Aliye London, Ben Rawlence (Kiingereza, Kiswahili): +44-79-8481-6013 (simu ya mkononi); ama rawlenb@hrw.org
Aliye New York, Elizabeth Evenson (Kiingereza): +1-917-428 1092; ama evensoe@hrw.org
Aliye New York, Daniel Bekele (Kiingereza, Amharic): +1-212-216-1223; or +1-917-385-3878 (simu ya mkononi); ama bekeled@hrw.org